Ajenda ya Watoto

The Children's Agenda

"Tuwape nafasi viongozi wanaojali watoto kwa kutetea haki zao" Baraza la Watoto

Zaidi ya nusu ya Watanzania ni watoto. Hivi sasa, kuwekeza kwa watoto kunanufaisha familia zetu, jamii zetu na ni kwa mustakbali wa Tanzania. Dira ya Tanzania inayostawi kiuchumi inaweza kufikiwa tu ikiwa watoto wetu watakua wakiwa na afya, wenye kupata lishe bora, elimu bora na kulindwa dhidi ya vurugu, udhalilishaji na unyonyaji.

Kila nchi iliyofikia kuwa na maendeleo ya kiuchumi ya kipato cha wastani imewekeza kwa watoto kwa kiwango kikubwa. Hivi sasa, kuwekeza kwa watoto kwenye elimu bora, huduma za afya zilizoboreshwa na kuwalinda watoto dhidi ya vurugu na udhalilishaji huzaa matunda yanayosababisha kuwepo kwa uchumi imara, kupungua kwa uhalifu na kuwepo kwa familia zenye afya bora.

Maendeleo makubwa yanaweza kupatikana kwa kuzihamasisha jamii zetu, kuongeza uwajibikaji na uwazi na kuhakikisha kuwa Sheria ya Watoto inatekelezwa kikamilifu ili kuwalinda watoto wetu. Matumizi mazuri ya rasilimali zilizopo kwa kuboresha huduma muhimu na kuimarisha fursa kwa watoto kutaziwezesha familia nyingi kujitoa kutoka kwenye umasikini.

1 Wekeza kuokoa maisha ya watoto na wanawake

Vifo vya watoto vimepungua kwa asilimia 25 na tunaendelea vizuri kuelekea kwenye Lengo la Maendeleo ya Milenia kuhusiana na uhai wa mtoto. Hata hivyo, zaidi ya watoto 445 walio chini ya umri wa miaka 5 hufa kila siku – na zaidi ya 140 kati ya hao ni wa umri chini ya mwezi mmoja.* Kila saa moja, kuna mwanamke anayekufa kwa kutokana na matatizo ya mimba au kujifungua. Kuwekeza kwenye huduma za afya nafuu kutaokoa maisha ya maelfu ya watu.

- Tunahitaji mfumo bora zaidi wa afya utakaokuwa na wafanyakazi zaidi, vituo vya afya vyenye vifaa vya kutosha, ufuatiliaji na usimamizi mzuri na uwajibikaji mkubwa. Sera, sheria, miongozo na miundo yote inayohusiana na afya, itoe kipaumbele kwa wanawake na watoto kwanza.
- Ni lazima tupanue uwekezaji katika huduma zisizo ghali ambazo hunusuru maisha. Lazima tuhakikishe kuwa:
  - ◊ Familia zote zinapatiwa vyandarua vyenye dawa ya kuua wadudu ya muda mrefu ili kupunguza malaria;
  - ◊ Watoto wote wanapatiwa chanjo za kujikinga na – magonjwa yanayozuilika;
  - ◊ Wazazi wote wanajua kuyatibu magonjwa hatari, kama vile kuharisha, kwa kutumia ORS na zinki;
  - ◊ Wazazi wote wanaelewa umuhimu wa kutowapa watoto kitu chochote isipokuwa maziwa ya mama mpaka wafikie umri wa miezi sita.
- Kila mmoja, pamoja na zile familia masikini kabisa, ataweza kapata huduma za afya. Kila mama lazima awe na fursa ya kujifungua kwa kuhudumiwa na mzalishaji mwenye ujuzi.
- Kamati za afya za jamii zifufuliwe ili kuhakikisha kuwepo kwa ushiriki na uwajibikaji wa jamii katika utoaji na ubora wa huduma za afya.

2 Wekeza kwenye lishe bora

Zaidi ya theluthi moja ya watoto wa Tanzania hawafikii kiwango chao cha ukuaji kimwili na kiakili kwa sababu ya

Watoto wakiwa Sehemu ya Watu wa Tanzania



Source: NBS 2006

Maeneo Kumi Muhimi ya Uwekezaji kwa Watoto

Maeneo kumi muhimu ya uwekezaji yamefafanuliwa kutokana na uchambuzi na mashauriano ya kina ikiwa ni pamoja na mashauriano na watoto wenyewe. Kuwekeza kwa watoto katika maeneo haya ya kipaumbele kunaweza kupunguza umasikini na kuwezesha kuwepo kwa taifa linalostawi na la usawa.

Maeneo kumi ya kipaumbele ni :

1. Wekeza kuokoa maisha ya watoto na wanawake
2. Wekeza kwenye lishe bora
3. Wekeza kwenye usafi, udhibiti wa miundombinu ya maji taka na ugavi wa maji katika shule na kwenye huduma za afya
4. Wekeza katika kumwendeleza mtoto akiwa bado mdogo
5. Wekeza kwenye elimu bora kwa watoto wote
6. Wekeza katika kuzifanya shule kuwa mahali pa usalama
7. Wekeza katika kuwalinda watoto wachanga na wasichana dhidi ya VVU
8. Wekeza katika kupunguza mimba za utotoni
9. Wekeza katika kuwanusuru watoto na vurugu, udhalilishaji na unyonyaji
10. Wekeza kwa watoto wenye ulemavu

* Inatokana na mtazamo wa makadirio ya watu la mwaka 2010 na kiwango cha vifo vya watoto walio chini ya miaka mitano 91 kwa wanaozaliwa hai 1,000 Utafiti wa viashirio vya VVU-UKIMWI 2007/8

utapiamlo. Utapiamlo unasababisha vifo zaidi ya theluthi moja vya watoto – inakadiriwa zaidi ya watoto 40,000 wa Kitanzania walio chini ya umri ya miaka mitano watapoteza maisha mwaka 2010 kwa sababu zinazohusiana na utapiamlo. Madhara makubwa hutokea wakati wa ujauzito na katika miaka miwili ya mwanzo ya maisha ya mtoto na hatua za kuchukuliwa ni lazima zilenge katika kipindi hiki cha maisha. Lishe bora kwa watoto na wanawake ni muhimu ili kuwa na uchumi imara. Mtazamo mpya unaolenga kwenye maendeleo ya kilimo umetoa fursa ya kufanya lishe bora iwe na umuhimu mkubwa katika maendeleo ya Tanzania.

- Vyakula rahisi vilivyorutubishwa lazima vipatikane kwa wingi nchini Tanzania. Sheria, kanuni na viwango husika ni lazima vipitishwe haraka na kuanza kutumika.
- Kila kituo cha afya kinapaswa kutoa huduma ya lishe bora kwa watoto na wanawake, hii ikiwa ni pamoja na ziada ya vitamini A na madini ya chuma, ushauri juu ya namna bora ya kulisha watoto na wanafamilia wengine na tiba ya utapiamlo.
- Kila Wilaya itenge bajeti na kuajiri mtaalamu wa mambo ya lishe bora ambaye atakuwa na dhamana ya kutoa huduma zinazohusiana na lishe bora kwa watoto na wanawake.
- Mtaalam wa lishe atasaidia kuelimisha familia kuhusu upangaji na utengenezaji chakula chenye lishe bora chenye mchanganyiko wa nafaka, mbogamboga, matunda na mazao yanayotokana na mifugo ili familia ziweze kufahamu mbinu bora za kuhifadhi na a kuwa na chakula chenye lishe bora kwa mwaka mzima.
- Mbinu za kunusuru maisha na fedha za huduma za jamii lazima ziwafikie wanawake wajawazito walio hatarini na watoto walio chini ya umri miaka miwili kuwawezesha kupata lishe bora.

3 Wekeza katika huduma bora za maji na usafi wa mazingira hasa vyoo shuleni na kwenye vituo vya afya

Katika kila shule tano, shule nne hazina huduma za kunawa mikono. Shule nyingi zina choo kimoja kwa zaidi ya watoto 50. Shule tatu katika kila shule tano hazina maji ya bomba. Sehemu nyingi za kutoa huduma ya afya zimo katika hali mbaya. Kuboresha afya na mifumo ya udhibiti wa maji taka shuleni kutapunguza maradhi, kutaongeza mahudhurio na kuhakikisha kuwa watoto, hasa wasichana, wanamaliza masomo yao. Maji ya bomba na vyoo katika sehemu zinazotoa huduma za afya ni muhimu katika kupunguza maambukizi ya magonjwa mbalimbali na kuokoa maisha.

- Shule zote zinapaswa ziwe na sehemu za kunawia mikono, vyoo, kufundisha somo la afya na ziwe za kiwango kinachotakiwa na serikali.
- Kila mradi wa maji unaopatiwa fedha kijijini lazima ujumuishe huduma ya maji shuleni na sehemu zinazotoa huduma za afya.
- Maji, udhibiti wa mifumo ya maji taka na huduma za usafi lazima ziboreshwe katika maeneo ya jamii masikini sana hasa katika maeneo ya mijini; hii inaweza kuwa ni pamoja na kutoa ruzuku kwa vibanda vya kuchotea maji na kuboresha huduma ya kupakua vyoo vya shimo.

4 Wekeza katika kumwendeleza mtoto akiwa mdogo

Mipango kwa ajili ya watoto wadogo ipo mstari wa mbele katika vita dhidi ya umasikini. Watoto katika jamii zilizo masikini sana wamo katika hatari kubwa za kupata maradhi na utapiamlo na hawafanyi vizuri shuleni. Mipango jumuishi ya watoto wadogo inayolenga watoto walio masikini sana huzisaidia familia kuwa na mwanzo mzuri wa watoto wao na husaidia kupunguza pengo kati ya masikini na matajiri. Uwekezaji kwa watoto wadogo una faida mara saba na una thamani kuliko kuwekeza kwenye mipango ya kunusuru maisha ya mtoto hapo baadaye.

- Wazazi fukara wapatiwe msaada wanaohitaji ili kuhakikisha kuwa watoto wao wanakuwa na mwanzo mzuri zaidi katika maisha. Msaada kwa ajili ya miradi ya kijamii ya kulea watoto na ya maendeleo na makuzi ya awali ya watoto itasaidia katika kuhakikisha kuwa watoto wanakua wakiwa na afya, wanapata lishe bora na wametayarishwa vizuri kwenda shule.
- Maendeleo ya watoto wadogo yaingizwe katika muhtasari wa mafunzo kazini ya walimu. . Yaanzishwe mafunzo kazini ya kitaifa kwa wote wanaohudumia watoto wadogo. Wale wanaofanya kazi katika jamii fukara wapewe kipaumbele katika mafunzo haya.
- Zianzishwe kamati za kijamii katika ngazi ya wilaya na kata ambazo zitafuatilia upatikanaji wa huduma na kusaidia uboreshaji wa vituo vya kumwendeleza mtoto akiwa mdogo.

5 Wekeza kwenye elimu bora kwa watoto wote

Ni zaidi kidogo ya nusu ya wanafunzi ndio wanaofaulu mtihani wa kumaliza shule ya msingi. Chini ya mtoto mmoja katika kila watoto kumi katika maeneo ya vijijini ndiye anayeandikishwa shule ya sekondari. Wahitimu wa shule walioelimika vizuri ni muhimu kwa maendeleo madhubuti ya kiuchumi. Mpango wa kitaifa wa mafunzo kwa walimu walio kazini unaweza ukabadili sana matokea mabaya ya shule ya hivi sasa.Ufundishaji shirikishi utaboresha uhusiano kati ya mwanafunzi na mwalimu na kuwatia motisha wanafunzi zaidi kumaliza masomo yao.

- Kwa kushirikiana na wahisani, inapasa kuongeza kiwango cha fedha kwa ajili ya elimu ya msingi na ya sekondari na hasa kwa ajili ya mafunzo, mishahara na motisha ya

walimu, , kuongeza vitabu, majengo ya shule na elimu isiyo rasmi.

- Matokeo ya shule yanaweza kuwa bora zaidi kwa kuunga mkono mpango wa mafunzo kwa walimu waliokazini. Hii itaanzisha utaratibu wa njia za kufundisha na kujifunza zinazomlenga mtoto na kupunguza msongamano darasani. Walimu wanaofanya kazi sehemu za mbali au mazingira magumu wapatiwe motisha.
- Ubora wa elimu unaweza kuboreshwa kwa kuanzisha ukaguzi wa kila mwaka wa shule zote. Uwajibikaji kwa walimu wakuu na walimu wengine wote uwe ni pamoja na mahudhurio, ukamilishaji wa kazi, utendaji bora na utumiaji wa njia za kufundisha zinazomlenga mtoto. Mambo haya yawe katika mfumo wa kawaida wa ufuatiliaji shuleni.

6 Wekeza katika kuzifanya shule kuwa mahali salama

Shule zinapaswa kuwa mahali salama kwa watoto. Wengi wamekuwa wakitishwa, kudhalilishwa na hivyo kuathiri uwezo wao wa kujifunza na kusababisha watoto wengi kuacha shule mapema. Kuwepo kwa michezo shuleni kunaweza kusaidia kupunguza vurugu na kuimarisha nidhamu, uhusiano kati ya mwanafunzi na mwalimu na kuongeza mahudhurio shuleni, ikiwa ni faida chache kati ya nyingi nyingine.

- Walinde watoto dhidi ya vurugu shuleni kwa kupitisha na kutumia sheria zinazopinga vurugu. Hakikisha kuwa wale wenye jukumu la kuwaweka watoto salama wanatimiza ahadi zao na kutekeleza wajibu wao.
- Saidia utaratibu wa kuanzisha mabaraza ya wanafunzi na kuwepo kwa wawakilishi wa wanafunzi waliochaguliwa katika utawala wa shule za msingi na za sekondari. Mabaraza ya shule huwawezesha wanafunzi kushiriki katika kutatua migogoro, kujifunza na kutumia haki zao pamoja na kujua wajibu wao kwa jamii nzima ya shule.
- Hakikisha kuwa watoto wana fursa ya kutoa taarifa kuhusu vurugu na udhalilishaji unaofanywa na wanafunzi wengine na walimu kwa namna ya usalama na kwa kujiamini. Hakikisha kuwa wale wanaohusika na vurugu na udhalilishaji, ikiwa ni pamoja na walimu na wanafunzi, wanawajibishwa.
- Ingiza michezo katika mitaala ya shule na katika mpango wa mafunzo ya walimu walio kazini.

7 Wekeza katika kuwalinda watoto wachanga na wasichana dhidi ya VVU

Maendeleo makubwa yamepatikana katika kupunguza kuenea kwa VVU. Hata hivyo, ambukizo moja katika kila maambukizo kumi mapya huwapata watoto wanaozaliwa japokuwa asilimia 90 ya maambikizi haya yangeweza kuzuilika. Wasichana pia wamo hatarini zaidi kuambukizwa VVU kuliko wavulana. Kila ambukizo jipya la kijana aliye chini ya miaka ishirini linadhihirisha kushindwa kuwapatia vijana elimu ya afya ya uzazi, taarifa, stadi na huduma zitakazowawezesha kujilinda. Unyanyapaa na ubaguzi vinaendelea kudhoofisha uwezekano wa wanawake kupata huduma.

- Fanya kazi pamoja na washiriki wote katika kupanua huduma na matibabu yatakayoangamiza kabisa maambukizi ya VVU ya mama kwa mtoto ifikapo mwaka 2015. Hakikisha kuwa watoto wote wenye VVU na UKIMWI wanapata matibabu wanayoyahitaji.
- Toa ahadi ya kuongeza rasilimali katika kuwakinga vijana, hasa wasichana dhidi ya VVU na UKIMWI kwa kuunga mkono mpango wa kitaifa wa kuzuia VVU.
- Saidia katika kuanzisha huduma za afya zinazowalenga vijana na mipango madhubuti ya stadi za maisha ambazo zitawapa taarifa na kuwawezesha, hasa wasichana kupunguza uwezekano wao wa kuambukizwa VVU na UKIMWI.

8 Wekeza katika kupunguza mimba za utotoni

Mnamo mwaka 2007 zaidi ya wasichana 8,000 waliacha shule kwa sababu ya mimba na idadi hii inaonekana kuzidi kila mwaka. Mimba za utotoni zinahatarisha mama vijana na watoto wao. Kupunguza mimba na kumhakikishia kila msichana haki yake ya kupata elimu ni muhimu katika vita dhidi ya umasikini

- Wasaidie wasichana kujilinda wenyewe kwa kuongeza maarifa yao juu ya mambo yanayohusu afya ya uzazi na tabia hatarishi. Hakikisha kuwa wavulana pia wanashirikishwa katika programu zenye madhumuni ya kupunguza mimba za utotoni.
- Saidia katika kupunguza umasikini kwa kuhakikisha kuwa shule zinaunga mkono na kutekeleza miongozo mipya inayowawezesha wasichana wenye watoto kuendelea na elimu yao.
- Ongeza wigo wa elimu ya ufundi kwa watoto wote walio nje ya shule. Kwa wasichana, hii inaweza kusaidia kupunguza umasikini na kuwa tegemezi kiuchumi, jambo ambalo mara nyingine huwaingiza katika tabia hatarishi.

9 Wekeza katika kuwanusuru watoto na vurugu, udhalilishaji na unyonyaji

Zaidi ya watoto milioni 2 ni yatima – wengine hulelewa na ndugu, wengine hupelekwa kwa jamaa na wengi huishia mitaani. Mamilioni ya watoto wamo katika hatari ya uwezekano wa kufanyiwa vurugu, kudhalilishwa na kunyonywa kwa nia ya kuwaingiza kwenye uhalifu. Hakuna mfumo madhubuti wa kulinda haki za watoto walio hatarini sana.

- Wekeza katika kuendeleza mfumo wa kuwalinda watoto wenye mwelekeo wa kutoa ulinzi wa kisheria, kubadili mwenendo wao na kuleta ustawi wa

jamii. Hakikisha kuwa polisi, wanasheria, majaji, wafanyakazi wa huduma za jamii, walinzi n.k. wamefunzwa vizuri kuzitumia sheria za watoto. Jamii inahitaji kuelewa jukumu na dhamana zao katika kuwalinda watoto katika jamii hizo.

- Wekeza katika huduma za watoto ambazo zitawalida wale walio katika mazingira hatarishi zaidi ikiwa ni pamoja na:
  - ◊ Msaada kwa familia zenye watoto wanaoishi katika umasikini ambao utasaidia katika kupunguza watoto kufanyishwa katika kazi ngumu na za uasherati na kupunguza idadi ya watoto wanaoishi katika vituo maalumu.
  - ◊ Huduma maalumu zinazohitajika kuwalinda na kukabiliana na udhalilishaji wa watoto. Hii ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa wafanyakazi wa huduma za jamii na washauri nasaha wa kutosha na wenye sifa ambao ni muhimu katika kuwashughulikia watoto waliofanyiwa ukatili.
- Watoto wote wanapaswa kuwa na vyeti vya kuzaliwa ambavyo vinalinda haki zao za kupata huduma muhimu na kusaidia kuwalinda dhidi ya kusafirishwa nje kibiashara na unyonyaji.
- Kuhakikisha mfumo wa sheria unawatendea watoto wanavyostahili na pale inapofaa, watolewe kutoka mchakato rasmi wa kisheria. Wekeza katika namna mbadala ya kuwazuia na kuwabadilisha tabia watoto waliofanya makosa na kupunguza hukumu ya kuwekwa jela. Mtoto asiwekwe gerezani pamoja na watu wazima.
- Hakikisha kuwepo kwa utoaji wa mara kwa mara hadharani wa takwimu zinazoonyesha hali ya watoto walio hatarini kutokana na udhalilishaji na unyonyaji na walio katika mfumo wa sheria za jinai.
- Hakikisha kuwa watoto wanaweza kushiriki katika utoaji maamuzi muhimu yanayohusiana na ustawi wao ikiwa ni pamoja na kubadilishwa kwa Baraza la Watoto kuwa chombo chenye uwakilishi wa kitaifa kinachoongozwa na watoto wenyewe.

10 Wekeza kwa watoto wenye ulemavu

Watoto wengi wenye ulemavu wananyimwa haki ya kupata elimu. Wengi hufungiwa ndani na kuwekwa katika hali za kinyama.

- Sheria zinazohusiana na watu wenye ulemavu zinapaswa kukamilishwa na kutekelezwa. Wahisani washirikishwe ili kuhakikisha kunakuwepo na bajeti kwa ajili ya utekelezaji, ikiwa ni pamoja na kuundwa kwa chombo cha uratibu.
- Upatikanaji wa huduma maalumu za watu wenye ulemavu unapaswa kuzidishwa, ikiwa ni pamoja na mipango ya jamii ya kuwawezesha kuishi maisha ya kawaida, vituo vya huduma na matibabu mahususi na kuwa na wafanyakazi waliopatiwa mafunzo ili watoto wote wenye ulemavu waweze kupatiwa huduma muhimu za kuwawezesha kuishi maisha ya kawaida, pamoja na vifaa wanavyohitaji.
- Ihakikishwe kuwa mipango yote na huduma, pamoja na shule, huduma za afya, usafiri na mawasiliano vinapatikana na kuwajumuisha watu wenye ulemavu wakiwa washiriki wakuu na wanufaikaji.

Photographs UNICEF/Julie Pudlowski

Kwa habari zaidi juu ya **Ajenda ya Watoto** wasiliana na:

childrensagenda@hotmail.com

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto
+255(0)22 2137679, +255(0)22 2132526
Katibu Mkuu na Idara ya Maendeleo ya Watoto

Dogodogo Center +255(0)222171575
Elizabeth Mwase

KIWOHEDE +255(0)754694107
Justa Mwaituka

CCBRT +255(022)2601543
Pennie Cabot, Suzan Boon

Caucus for Children's Rights
+255(0)787703334
Kate McAlpine

PLAN International +255(0)222773264
Wilbert Muchunguzi

Right to Play +255(0)222774161
Godfrey Boniphace

Save the Children +255787810215
Derrick Mbelwa

UNICEF +255(0)222196600
Sara Cameron

Voluntary Service Overseas
+255(022)2600053
Betty Malaki

World Vision +255(0)222775224
Esther Mongi

Association of Journalists Against AIDS in Tanzania (AJAAT)
+255(0)75410655 George Nyembela

TENMET +255(0)22 2150793
Anthony Mwakibinga